**Viwango vya Chini vya Utendakazi**
**(MOS)**

# Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma na Wafanyakazi wenyewe (MOS-PSEA)[1]

Tafsiri hii imeandaliwa na Social Development Direct na Translators without Borders kwa kusudi la kuhabarisha tu. Usahihi wake hauwezi kuhakikishwa na Kamati ya Kudumu ya Umoja wa Mawakala (Inter-Agency Standing Committee /IASC). Toleo rasmi la pekee ni maandishi ya Kiingereza yanayopatikana kwenye tovuti ya Kamati ya Kudumu ya Umoja wa Mawakala (IASC) kupitia linki ifwatayo: Minimum Operating Standards - Protection from Sexual Exploitation and Abuse by own Personnel.

Ili kutoa Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma (PSEA) na wafanyakazi wenyewe kufuata Viwango vya Chini vya Uendeshaji kwa Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma (MOS-PSEA) vinahitajika. Viwango vya Chini vya Utendakazi kwa Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma (MOS-PSEA) imeigwa baada ya utaratibu wa kufuata unaojulikana sana wa Viwango vya Chini vya Uendeshaji wa Usalama kwa Usalama wa Wafanyakazi (au MOSS), ambao ni lazima kwa Mfumo wa Umoja wa Mataifa (UN) kuhakikisha kuwa kuna mahitaji ya kawaida ambayo mashirika yote hufuata ili kuhakikisha usalama wa wafanyakazi.

## MOS-PSEA ni nini?

MOS-PSEA vinategemea:

1. Tamko la Kujitolea juu ya Kukomesha Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma na Wafanyakazi wa Umoja wa Mataifa na Wasio wa Umoja wa Mataifa, Agosti 2008
2. Mapitio ya Ulimwenguni ya Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma na Umoja wa Mataifa, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Shirika la Uhamiaji la Kimataifa na Wafanyakazi wa Shirikisho la Kimataifa la Msalaba Mwekundu, Julai 2010
3. Kanuni Kuu Sita za Kamati ya Kudumu Kati ya Mashirika (IASC) zinazohusiana na Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma, Juni 2002

## Je! Ni vipi vipengere muhimu vya Viwango vya chini vya Uendeshaji kwa Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma MOS-PSEA?

Nguzo nne za kazi ya sasa ya Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma PSEA hutoa mfumo wa utaratibu. Hizi ni:

1. **Usimamizi na uratibu:** Uundaji bora wa sera na utekelezaji; Mipango ya ushirika; Idara Maalum /Mratibu wanao wekwa kwa Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma PSEA.
2. **Kujihusisha na kuunga mkono jamii ya watu wa eneo husika:** Mawasiliano bora na kamili kutoka Makao Makuu (HQ) kwenda ngazi za utekelezaji juu ya (a) nini cha kufanya kuhusu kuongeza uelewa wa walengwa juu ya Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma PSEA na (b) jinsi ya kuanzisha njia madhubuti za malalamiko ya jamii.
3. **Kuzuia:** Njia madhubuti na kamili za kuhakikisha uhamasishaji juu ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma SEA kati ya wafanyakazi; ajira bora na usimamizi wa utendaji.

4. **Mwitikio:** Malalamiko ya ndani na taratibu za uchunguzi zimewekwa.

---

[1] Hivi Viwango vya Chini vya Utendakazi vimejadiliwa kati ya Wanachama wa Kikosi Kazi (TaFo) cha Kamati ya Kudumu Kati ya Mashirika (IASC) ya Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma (PSEA); hati hii ni kazi inayoendelea na inaonyesha hali ya mawazo ya sasa ya Kikosi Kazi.

| | Viwango vya Chini vya Utendakazi kwa Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma | Viashiria Muhimu |
|---|---|---|
| 1 | **Ufanisi wa Kubuni Sera na Utekelezaji** | ● Sera inayo elezea viwango vya mwenendo, pamoja na matendo ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma SEA, ipo na mpango kazi wa kutekeleza sera hiyo upo tayari.<br>● Sera hiyo/viwango vya mwenendo vimewasilishwa kwa wafanyakazi wa sasa na menejimenti kuu (katika Makao Makuu (HQ) na ngazi za utekelezaji) mara kwa mara (kama vile makati wa kuingizwa na mafunzo mapya). |
| 2 | **Mipangilio ya Ushirika** | ● Taarifa Rasmi ya Habari ya SG (ST/ SGB/2003/13) au kanuni husika zime jumuishwa katika hali ya mkataba wa jumla.<br>● Taratibu zipo za kupokea makubaliano ya maandishi kutoka kwa mashirika au watu wanaoingia katika mipango ya ushirika na shirika ambalo wanalijua na watatii viwango vya sera ya Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma PSEA. |
| 3 | **Idara/mratibu maalum wamewekwa kwa Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma PSEA** | ● Idara/mratibu maalum wana jukumu la jumla kwa maendeleo na utekelezaji wa sera na shughuli za Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma PSEA.<br>● Idara inayo husika/mratibu maalum wanahitajika kuripoti mara kwa mara kwa wasimamizi waandamizi juu ya maendeleo yao juu ya Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma PSEA kupitia Mratibu Mwandamizi wa Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma PSEA.<br>● Wafanyakazi wanao shughulika na Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma PSEA wana majukumu rasmi kwa Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma PSEA katika maelezo yao ya kazi, tathmini ya utendaji au sawa na hayo.<br>● Wamepata mafunzo ya mfumo juu ya Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma (PSEA) na wakati uliowekwa kwa Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma (PSEA) ni sawa na kiwango cha utekelezaji kinacho hitajika chini ya hali ya sasa ya shirika. |

| | Viwango vya Chini vya Utendakazi kwa Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma | Viashiria Muhimu |
|---|---|---|
| 4 | **Mawasiliano bora na kamili kutoka Makao Makuu (HQ) kwenda ngazi za utekelezaji juu ya matarajio juu ya kuongeza uelewa wa walengwa kuhusu Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma PSEA** | ● Makao Makuu (HQ) yame wasilisha kwa kina matarajio kuhusu juhudi za kuongeza uelewa wa walengwa kuhusu Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma PSEA (pamoja na habari juu ya viwango vya mwenendo wa shirika na utaratibu wa kuripoti).<br>● Makao makuu (HQ) yame sambaza mifano ya zana za kuongeza ufahamu na vifaa vya kutumiwa kwa shughuli za kuongeza uelewa wa walengwa. |
| 5 | **Mifumo madhubuti za malalamiko ya jamii (CBCM), pamoja na msaada wa waathirika.** | ● Makao Makuu (HQ) yanataka ofisi zake ngazi za utekelezaji kushiriki katika mifumo ya malalamiko ya jamii ambayo inaundwa na kutekelezwa kwa pamoja na jamii ya misaada iliyo rekebishwa kwa maeneo hayo.<br>● Kuna mwongozo uliotolewa kwa ngazi za utekelezaji kuhusu jinsi ya kubuni mifumo ya malalamiko ya jamii (CBCM) ili kuhakikisha ina rekebishwa kwa muktadha wa kitamaduni kwa kuzingatia ushiriki wa jamii.<br>● Kuna utaratibu wa ufuatiliaji na uhakiki wa utaratibu wa malalamiko.<br>● Shirika lime andika mwongozo juu ya utoaji wa msaada wa waathirika. |
| 6 | **Uajiri mzuri na usimamizi wa utendaji** | ● Shirika lina hakikisha kuwa wagombea wote wana takiwa kusaini kanuni za maadili kabla ya kupewa kandarasi.<br>● Kila shirika lina jitolea ku boresha mfumo wake wa kuangalia kumbukumbu na kukagua utovu wa nidhamu wa awali.<br>● Usimamizi na tathmini ya utendaji ni pamoja na kuzingatia ushiriki katika Mafunzo ya Kanuni za Maadili (au sawa yake) ambayo ni pamoja na Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma PSEA.<br>● Tathmini ya utendaji kwa Wasimamizi Waandamizi ni pamoja na uzingatiaji wa kuunda na kudumisha mazingira ambayo yanazuia unyonyaji wa kijinsia na dhuluma inakuza utekelezaji wa ST/SGB/2003/13 au kanuni za maadili. |

| | Viwango vya Chini vya Utendakazi kwa Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma | Viashiria Muhimu |
|---|---|---|
| 7 | **Mifumo madhubuti na kamili imewekwa ili kuhakikisha uhamasishaji juu ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma (SEA) kati ya wafanyakazi** | ● Wafanyakazi hupokea mafunzo mapya kila mwaka juu ya viwango vya mwenendo, hujifunza juu ya utaratibu wa kuwasilisha malalamiko na ripoti za utovu wa nidhamu na athari za kukiuka viwango hivi.<br>● Mafunzo juu ya utovu wa nidhamu haswa tuki taja Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma SEA ni sehemu ya mchakato wa kuingizwa.<br>● Wafanyakazi wanajua wajibu wao wa kuripoti Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma (SEA) / utovu wa nidhamu na wanajua kuwa kuna sera ya Ulinzi kutoka kwa kisasi kilichopo. |
| 8 | **Malalamiko ya ndani na taratibu za uchunguzi zipo** | ● Taratibu zilizoandikwa juu ya malalamiko/ripoti za utunzaji kutoka kwa wafanyakazi au walengwa zipo.<br>● Wafanyakazi wana julishwa mara kwa mara jinsi ya kuwasilisha malalamiko/ripoti na taratibu za kushughulikia haya.<br>● Taratibu za kawaida za uchunguzi au sawa na hizo zinazo tolewa na kutumika kuongoza mazoezi ya uchunguzi.<br>● Uchunguzi una fanywa na wataalamu wenye ujuzi na walio hitimu ambao pia wamefundishwa juu ya uchunguzi nyeti kama vile madai ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma (SEA).<br>● Uchunguzi umeanza ndani ya miezi 3 na habari juu ya mafanikio yata shirikiwa na mlalamikaji.<br>● Malalamiko yaliyo thibitishwa yame sababisha hatua za kinidhamu au matokeo ya kandarasi na, ikiwa siyo hivyo, taasisi hiyo ina uwezo wa kuhalalisha kwa nini isiwe hivyo. |